

# CHUO KIKUU CHA DAR ES SALAAM

S.L.P. 35091 ♦ DAR ES SALAAM ♦ TANZANIA

OFISI YA MAWASILIANO NA HABARI



## TAARIFA KWA UMMA

Zanzibar, Oktoba 4, 2021

### Maabara ya Muda Kujengwa IMS Kuwezesha Kuanza Mwaka wa Masomo

Serikali imeazimia kujenga maabara ya muda kwa ajili ya Taasisi ya Sayansi za Bahari (IMS), Zanzibar, ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ili kukidhi mahitaji ya ufundishaji na utafiti wakati utapoanza mwaka wa masomo 2021/22 mwishoni mwa mwezi Oktoba mwaka huu, baada ya maabara iliyokuwepo kuteketea kwa moto.

Maazimio hayo yametolewa na Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Mhe. Prof. Joyce Ndalichako (Mb.), baada ya kutembelea na kujionea madhara yaliyotokana na ajali ya moto iliyotokea katika jengo la Taasisi hiyo lililokuwa na maabara hiyo lililopo Mizingani, Bandarini, Zanzibar.

Waziri Ndalichako amesema kuwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itahakikisha inafanya kila liwezekanalo ili mazingira kwa ajili ya masomo na tafiti yarejee kama ilivyokuwa awali na kuwawezesha wanafunzi na wanataaluma wa Taasisi hii kuendelea na ratiba zao kama kawaida.

Aidha, Waziri Ndalichako aliambatana na Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Mhe. Simai Mohamed Said ambaye alisema kwamba, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, yeye mwenyewe na wadau wengine watatoa msaada unaohitajika, na kufuatilia kwa karibu ukarabati na upatikanaji wa maabara na vifaa husika.

“Taasisi ya Sayansi za Bahari Zanzibar ni kitovu cha Uchumi wa Bluu ambao ni kati ya vipaumbele vikubwa vya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar chini ya Rais Hussein Mwinyi; hivyo tutahakikisha tunanunua vifaa vingine vya maabara”, alisema Mhe. Said.

Naye Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Prof. William Anangisye alitoa shukrani kwa Serikali, vyombo vya ulinzi na usalama na wananchi kwa kujitua kwa nguvu zote kuhakikisha moto unadhibitiwa kabla haujaleta madhara makubwa zaidi katika Taasisi hii inayotoa masomo ya Shahada za awali na uzamili. Pia, Prof. Anangisye alimhakikikishia Waziri Ndalichako kuwa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kitatekeleza maazimio haya; na kuwasihi wanafunzi na wanataaluma wawe watulivu katika kipindi hiki.

Jengo hili la Taasisi ya Sayansi za Bahari liliungua moto siku ya Jumamosi tarehe 2 Oktoba 2021, ambapo, kwa mujibu wa Mkurugenzi wa Taasisi ya Sayansi za Bahari, Dkt. Magreth Kyewalyanga vyumba vyote vitatu vya maabara na vifaa vyote vilivyokuwemo viliteketea.

“Pia vyumba vingine sita yaani madarasa matatu ya wanafunzi wa uzamili, ofisi mbili na chumba cha server, ambavyo vilikuwa na vifaa vya maabara na samani mbalimbali za ofisi vimeteketea”, amesema Dkt. Kyewalyanga. Hata hivyo, Dkt. Kyewalyanga ameeleza kuwa chanzo cha moto na hasara halisi bado havijathibitishwa, na vinafanyiwa kazi na vyombo husika vya dola.

Viongozi wengine waliofika katika ziara hii ni pamoja na Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Profesa James Mdoe, Naibu Makamu Mkuu wa Chuo – Taaluma, Profesa Bonaventure Rutinwa, na Mratibu wa Shughuli za Serikali, Ofisi ya Makamu wa pili wa Rais, Bw. Khamis Ahui na viongozi mbalimbali.





